

327.2 E78.2 *The Epistle to the Romans*  
*(Suaahili)*  
SL III La

HC 8748

WARAKA WA PAOLO MTUME

Cambridge University Library  
www.lib.cam.ac.uk/is  
KWA

WARUMI.

SO  
Cambridge University Library  
LI  
www.lib.cam.ac.uk/is  
DEO  
GL  
OR  
IA

327.2 E78.2

ZANZIBAR:

1878.  
Cambridge University Library  
www.lib.cam.ac.uk/is

K



9002302096 ✓

EMUTM QLOI BLOO KARAV

Cambridge University Library  
www.lib.cam.ac.uk/is

WARUM



Cambridge University Library  
www.lib.cam.ac.uk/is

OF  
17



Cambridge University Library  
www.lib.cam.ac.uk/is



17  
17



WARAKA WAKE PAOLO MTUME

KWA

WARUMI.

**P**AOLO mtumwa wa Isa Masiya aliyelitwa kuwa mtume, aliyewekwa kwa anjili ya 2 Muungu, aliyohidi kwa nabii zake katika 3 maandiko matakatifu, ya Mwana wake, aliye 4 kwa mwili wa wazao wa Daud, akapambanuka kuwa Mwana wa Muungu kwa uwezo kwa roho ya utakatifu katika ufufuo wa 5 wafu, Isa Masiya, Bwana wetu, naye yule tukapewa neema na utume, kwa kusikiwa imani katika mataifa yote kwa jina lake. 6 Katika hawa mme kuwa na ninyi, mmeitwa 7 na Isa Masiya. Wote walioko katika Rumi, waliopendwa na Muungu, walioitwa watakatifu, neema kwenu na amani kwa Muungu Baba wetu naye Bwana Isa Masiya. 8 Kwanza namshukuru Muungu wangu kwa Isa Masiya kwa ajili yenu nyote, kwamba imani yenu inahubiriwa ulimwenguni



## KWA WARUMI. I.

Cambridge University Library

- 9 mwote. Muungu ni shahidi wangu nimwabu-  
buduye rohoni katika anjili ya Mwana wake,  
kama pasipo kukoma nawanena sikuzote,  
10 dayima katika sala zangu naomba, kama  
hatta sasa nipate kusafiri vema kwa mape-  
11 nzi ya Muungu kuja kwenu. Kwani nata-  
mani kuwaona, nipate kuwaletea ukarimu  
12 wa rohoni, mfanyike imara, ndivyo nipate  
kufarijiana nanyi kwa imani yenu na yangu.  
13 Sitaki msijue, ndugu, kama marra nyingi  
nimeshika kuja kwenu nikazuiliwa hatta  
sasa, nipate matunda kwenu kama katika  
14 mataifa yaliyosalia. Wayonani na wangineo  
15 wenyi hekima na wasio kufikiri waniwia.  
Hivi nia yangu kuhubiri anjili na kwenu  
katika Rumi.  
16 Kwani sitahayariki na anjili, ndiyo ngu-  
vu ya Muungu kwa wokovu wake killa aa-  
miniye, Myahudi kwanza, tena Myonani.  
17 Kwani haki ya Muungu imethihirika na-  
yo katika imani hatta imani, kama ilivyoa-  
ndikwa, Mwenyi haki ataishi kwa imani.  
18 Hasira ya Muungu katika mbinguni ime-  
funuka juu ya unajisi wote na thulumu ya

Cambridge University Library

www.lib.cam.ac.uk/is



## KWA WARUMI. I.

- 19 watu walio nayo kweli pasipo haki. Kwani  
iliyojulikana ya Muungu imekuwa wazi  
20 kwao, kwani Muungu amewaonyesha. Kwani  
yasiyoonekana yake tangu kuumbwa uli-  
mwengu yameonekana kwa akili katika viu-  
mbe, kama uwezo wake na umuungu usioo-  
21 nekana. Hatta hawana neno la kutoa, kwa  
sababu wakimjua Muungu hawakumsifu  
kama Muungu wala hawakumshukuru, illa  
wakabatilika katika majadiliano yao, moyo  
22 wao wa barathuli ukaona giza; wakijinena  
23 wenyi hekima wamepumbazika, wakabadili  
sifa zake Muungu asiyeharibika kuwa mfa-  
no wa sanamu ya mtu aharibikaye, nao we-  
nyu mabawa, nao wenyi miguu minne, nao  
watambaao.
- 24 Kwa hiyo Muungu akawatoa kwa tamaa  
za mioyo yao katika uchafu, waharibiane  
25 heshima ya miili yao. Waliobadili kweli  
ya Muungu kuwa uwongo, wakasujudia  
wakaabudu kiumbe kuliko muumba aliye-  
barikiwa milele. Amina.
- 26 Kwa hiyo Muungu amewatoa wapatwe  
na aibu. Hatta waanaake wao wakabadili



## KWA WARUMI. II.

Cambridge University Library

27 tumio la asili kwa lile lisilo la asili. Kama  
na waume, wakiacha tumio la mke la asili,  
wakawaka na tamaa wao kwa wao, waume  
wakifanya na waume yasiyosulihi wakapo-  
kea wenyewe thawabu yaliyoistahilia mako-  
sa yao.

28 Na kama hawakukubali kumshika Muu-  
ngu kwa akili, akawatoa Muungu kwa moyo  
29 usio na akili, wayafanye yasiyofaa. Waka-  
jawa na thulumu yote, ubaya, kutamani, u-  
ovu, wakajaa hasidi, naji, fitina, hila, ubaya,  
30 waambao, wasingiziao, wachukia Muungu,  
wenyi jeuri, wenyi kiburi, wajisifuo, watu-  
31 ngao maovu, wawaasio wazee, wasio na akili,  
wavunjao ahidi, wasiopendana, wasiohuru-  
32 mia. Waliojua hukumu ya Muungu kama  
wayafanyao haya wamestahili kufa, hawaya-  
fanyi tu, illa wamependezewa nao wayafa-  
nyao.

II. Kwa hiyo huna neno la kutoa, ee killa  
mtu uhukumuye, kwani ukimhukumu mwi-  
ngineo umejihukumu mwenyewe, kwani u-  
2 hukumuye wayafanya yaleyale. Twajua  
kama hukumu ya Muungu ni kwa kweli juu

Cambridge University Library

www.lib.cam.ac.uk/is